# Je, Wewe ni Shujaa Katika Uangalizi wa Mafuta, Gesi Asilia na Madini?

# Je, Unaleta Ufanisi Katika Mpango wa Uwazi wa Sekta ya Nishati na Madini (EITI) ?



**"Tunajiunga na taasisi hii ili kuongeza na kupanua wigo wa kudhibiti rasilimali za madini, si kwamba kwa sasa hatuwezi, tunachokifanya ni kuunganisha nguvu zetu kama taifa na zile za kimataifa."**

*Mh. William Ngeleja - Waziri wa Nishati na Madini(2008-2012)*
*(Mwananchi, limewekwa kwenye tovuti Nov. 21/2008 - www.mwananchi.co.tz/newsrids.asp)*

## Je, tunafahamu nini kuhusu mapato yatokanayo na mafuta, gesi asilia na madini?

Mapato ya serikali yanayotokana na sekta ya mafuta, gesi asilia na madini mara nyingi hufichwa na mwamvuli wa usiri unaotoa mwanya wa kushamiri ufisadi na usimamizi mbaya.

Kwa raia wa kawaida kufaidika, na nchi kukua, lazima taarifa zifichuliwe kuhusu kiasi gani cha pesa kinazalishwa na kinaenda wapi. Uwazi kama huu wa mapato ni muhimu sana kwa wabunge ili kuhakikisha kuwa mapato yanatumika kwa faida ya majimbo yao, na kwa ujumla, nchi nzima.

## Mpango wa Uwazi wa Sekta ya Nishati na Madini (EITI) ni Nini na Utakusaidiaje?

Mpango wa Uwazi wa Sekta ya Nishati na Madini (Extractive Industries Transparency Initiative, kwa kifupi EITI) huweka viwango vya kimataifa vya uwazi wa mapato katika sekta ya mafuta, gesi asilia na madini. EITI huzitaka nchi wanachama kufanya yafuatayo:

- Makampuni husika kuchapisha kiasi inachoilipa serikali.
- Serikali ichapishe kiasi inachopata kutoka kwenye makampuni husika.
- Msimamizi huru alinganishe taarifa hizi.
- Takwimu za mapato na hitilafu zake lazima zichapishwe katika 'ripoti za EITI'.
- Mchakato usimamiwe na Kamati ya Wadau Mseto ambayo lazima iwe na wajumbe kutoka serikalini, makampuni husika na asazi za kiraia.

Tanzania ndio kwanza imejiunga na EITI. Kwahiyo EITI ni chombo muhimu ambacho wabunge wanaweza kukitumia kuhakiki mapato inayopata serikali kutoka makampuni ya uchimbaji na uvunaji wa rasilimali za mafuta, gesi asilia na madini. Taarifa hizi ni muhimu ili kuelewa kiasi kinachozalishwa na uchimbaji huu, na kuhakikisha kuwa kinatengwa inavyostahiki katika mchakato wa bajeti.

## Unawezaje kuongoza katika kutia msukumo?

Mpango wa EITI ni wa kimataifa unaowezesha nchi zinazoutekeleza kupata sifa na kujulikana

kimataifa. Wabunge wanaowajibika katika EITI hupata nafasi ya kuwa sauti inayoongoza katika utawala bora na uwazi wa kiwango cha kitaifa na kimataifa.

## Kushiriki katika EITI

Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya jinsi unavyoweza kujifunza na kushiriki katika EITI:

- Pata taarifa fupi au warsha juu ya EITI kutoka serikalini.
- Hudhuria makongamano yanayoandaliwa na mashirika yanayosaidia EITI.
- Tembelea nchi inayotekeleza EITI ambako wabunge wanashiriki katika EITI.
- Fanya kazi na kamati maalum kufuatilia na kuangalia kazi za EITI.
- Pata taarifa ya utekelezaji wa EITI kutoka serikalini.
- Shirikiana na vyombo vya habari kuhamasisha umma na ainisha maeneo ambayo mchakato mzima unaweza kuboreshwa.
- Pata taarifa kuhusu EITI kutoka kwenye makundi ya asasi za kiraia na wataalam waliobobea katika kufuatilia sekta ya nishati na madini.
- Wasilisha jimboni ushiriki wako katika EITI ili kuleta mwamko wa jimbo na kuonesha jinsi uwazi na mpango wa EITI unavyowaletea mafanikio.
- Uwe mshauri na mchangiaji kwa wabunge kutoka nchi zingine zinazohitaji mwongozo kuhusu EITI.

## Wajibu wa Bunge Katika EITI

Katika baadhi ya nchi kama vile Kazakhstan na Mauritania, wabunge ni wajumbe wa Kikundi cha Wadau Mseto. Nchi zingine, kama Ghana, Wabunge wameamua kuwa na wajibu wa kusimamia masuala ya nje. Kwa Tanzania, wabunge kwa sasa hawawakilishwi katika kamati ya EITI lakini wanaweza kusimamia masuala ya nje au wakaomba kujiunga na kamati ya EITI.

Bunge lenye ufanisi ni muhimu ili kurekebisha mpango wa EITI na kuufanya uwe na mafanikio. Sheria na kanuni za EITI hutoa fursa pana ili kukidhi mahitaji ya kitaifa na ngazi za chini. Wabunge wanaweza kushiriki katika mchakato wa kurekebisha EITI ili kuhakikisha kuwa unafaa na kuwa na tija katika kushughulikia mahitaji ambayo ni mahsusi kwa Tanzania.

Baadhi ya mabunge, kama ya Nigeria na Liberia, yamepigania kuundwa kwa sheria za EITI. Sheria hizi hudhibiti utendaji na utekelezaji wa kuufanya mpango wa EITI uwajibike kwa Bunge.

## Tanzania na EITI

Tanzania ilijiunga na EITI Februari 2009. Wizara ya Nishati na Madini husimamia utekelezaji. Serikali ilikuwa na miaka miwili tu ya kutekeleza kikamilifu awamu moja ya mpango huu na kisha ifanyiwe mchakato wa tathmini huru, jambo ambalo husaidia kukidhi vigezo vya EITI. Kushindwa kukamilisha vigezo vyote vya uhalali huu ifikapo Februari 15, 2011 kumesababisha muda kuongezwa hadi 2012.Kushindwa tena kunaweza kuleta matokeo mabaya kwa hadhi ya nchi na kuathiri michango ya wahisani kwenye bajeti ya Taifa.

## Jifunze Zaidi Kuhusu EITI

Taasisi ya Usimamizi wa Mapato (Revenue Watch Initiative – RWI) imechapisha Mwongozo kwa Wabunge kwa kushirikiana na EITI, ambao unaambatana na taarifa hii fupi. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti zifuatazo:

Revenue Watch Institute:
*www.revenuewatch.org*

Extractive Industries Transparency Initiative:
*www.eitransparency.org*

Kama unataka kujua zaidi kuhusu EITI nchini Tanzania, tafadhali wasiliana na:

- Bw. Bubelwa Kaiza (mjumbe wa Asasi za Kiraia, Kamati ya EITI), *bubelwa.kaiza@fordia.org*
- Askofu Munga (mjumbe wa asasi za kiraia, Kamati ya EITI), *m5420@ail.trekia.se*
- Bw. Benedict Mushingwe (mjumbe mteule wa serikali kuhusu EITI), *mushingwe@yahoo.com*
- Ofisi ya Sekretalieti ya Policy Forum
  *info@policyforum.or.tz*

policy forum

Imechapishwa na Policy Forum.
S. L. P. 38486, Dar es Salaam, TANZANIA Simu: (255 22) 2780200
Simu ya Kiganjani: +255 782 317434, Barua pepe: info@policyforum.or.tz Tovuti: www.policyforum.or.tz

© Policy Forum 2009 na kuchapwa tena 2012